

## Maswali

1. Yesu alizungumza na watu wa aina gani?
2. Yesu alitaka watu wote wajue nini?
3. Yesu alisema mfano juu ya nini?
4. Mchungaji alisabua kondoo akapata wako tisini na tisa. Mmoja alikuwa amepotea. Alifanya nini?
5. Baadaye mchungaji alifanya nini?
6. Mbona mchungaji aliwaita pamoja marafiki wake?
7. Baadaye Yesu aliwambia hadithi ya mwanamke aliyepoteza shilingi moja. Alifanya nini?

## Majibu

1. Yesu alizungumza na watu wa aina tofaut tofauti.
2. Yesu alitaka kila mtu ajue juu ya upendo wa Mungu.
3. Yesu alisema mfano juu ya mchungaji aliyekuwa amepoteza kondoo mmoja.
4. Mchungaji alitafuta kila pahali mpaka akampata.
5. Baadaye alimweka kondoo juu ya mabega na akarudi nyumbani.
6. Mchungaji aliwaita marafiki waje ili, "Wafurahi."
7. Mwanamke huyo alitafuta shilingi yake moja iliyopotea mpaka akaipata.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM



### Awamu ya 1 Mwaka wa 2

# 42 Kondoo aliyepotea na shilingi iliyopotea

## Marejeo

Luka 15:4—10

## Kiini cha somo

Kuthibitisha kwamba Mungu anatupenda na wakati wote ako tayari kutusamehe makosa yetu tukitubu kwa kweli.

## Maneno maalum

1. Linganisha + wenye dhambi tubu + Mafarisayo
2. Watu tofauti + upendo wa Mungu
3. Kondoo 100 + mmoja amepotea
4. 99 salama + endelea kutafuta + pata aliepotea
5. Majirani + sifu Mungu
6. Furaha mbinguni + mwenye dhambi atubu
7. Hakuna dirisha + sakafu ya mchanga
8. Shilingi 10 + moja imepotea
9. Sifu Mungu
10. Mungu anaangalia na analinda

## KONDOO ALIYEPOTEA

**42.1** Yesu anatuonyesha wajibu na furaha yake kwa mwenye dhambi akitubu. Analinganisha na Mafarisayo na walimu wa sheria waliodhani kwamba hakuna haja ya kutubu.

**42.2** Yesu alizungumza na watu wa aina tofauti tofauti – tajiri, maskini, vijana, wazee, wachungaji na kama kawaida Mafarisayo na walimu. Yesu alitaka watu wote wajue juu ya upendo wa Mungu.

**42.3** Yesu aliwauliza swali, “Iwapo ulikuwa na kondoo mia moja na mmoja akapotea, utawaacha tisini na tisa na uende kutafuta aliyepotea mpaka umpate?”

**42.4** Baadaye aliwambia hadithi juu ya mtu aliyekuwa na kondoo mia moja na kwa sababu alikuwa akiwahesabu kila jioni, akapata kuwa mmoja hayuko. Aliwaweka tisini na tisa vizuri ndani ya kipanda na akaenda kutafuta aliyepotea. Alitafuta huku akimuita. Mwishowe alimpata huyo kondoo aliyepotea. Kwa furaha alimueka mabegani na kuenda nyumbani.

**42.5** Aliwaita pamoja marafiki na majirani wake na akasema, “Tumsifu Mungu, nimepata kondoo wangu aliyepotea.”

**42.6** Yesu alisema, “Nawambia kwamba, hivyo ndivyo furaha iko mbinguni kwa mwenye dhambi mmoja akitubu kuliko tisini na tisa waliohaki na hawataki kutubu.



## SHILINGI ILIYOPOTEA

**42.7** Nyumba za mashariki za wakati huo, hazikukuwa na madirisha na sakafu zilikuwa za mchanga. Kwa hivyo ilikuwa vigumu kutafuta shilingi moja

**42.8** Yesu aliwambia hadithi nyingine. “Iwapo kuna mwanamke aliyekuwa na shilingi kumi za fedha na akapoteza moja. Hatatafuta kimakini mpaka aipate?” Akiipata, atawaita pamoja marafiki na majirani wake waje akisema, “Tufurahi pamoja nimepata shilingi yangu iliyopotea.”

**42.9** Yesu alimaliza hadithi hii kama alivyomaliza ya kwanza. Kule mbinguni kuna sifa kuu kwa Mungu kwa mwenye dhambi mmoja anayetubu.

**42.10** Hizi hadidhi zote mbili zinatunyeshwa vile Mungu anatamani sana sisi tuwe watoto wake. Kama vile mchungaji alivyotafuta kondoo aliyepotea na mwanamke alivyotafuta shilingi iliyopotea ndivyo hivyo Mungu naye hutuungalia na anatulinda. Kunakuwa na furaha nyingi mbinguni wakati mmoja wetu anapoomba msamaha kwa Mungu na kuacha maovu ili amfuate.

